JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

# TAARIFA YA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA KWA TUME YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU WAKATI WA KIKAO CHAKE CHA 71.

**Nambari ya Mwanachama Hadhi Shirikishi. 14.**

**Jaji (Mst) Mathew P. M. Mwaimu.**

## 1.0 Salamu/ Itifaki

Waheshimiwa wajumbe wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; wanachama shirikishwa; wajumbe mliohudhuria Mkutano huu wa 71, pokeeni salamu za dhati kutoka kwa Serikali na watu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na salamu mahsusi na za kipekee kutoka kwa Makamishna na Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Tanzania (THBUB).

## 2.0 Sheria Iliyoanzisha Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni Idara huru ya Serikali iliyoanzishwa Mwaka 2001 kwa ajili ya kulinda, kukuza na kuhamasisha hifadhi ya haki za binadamu na misingi ya Utawala bora nchini Tanzania. Ni Taasisi ya Muungano iliyoanzishwa mwaka 2001 chini ya Ibara ya 129 (1) ya Katiba ya Nchi. Mamlaka ya Tume yametamkwa chini ya Ibara ya 130 (1) ya Katiba ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6 (n 1) cha Sheria ya THBUB [Sura ya 391]. Majukumu yake makuu ni kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini. Tume ilianza kufanya kazi rasmi tarehe 1 Julai, 2001 baada ya kuanza kutumika kwa Sheria Sura ya 391 na kuzinduliwa rasmi Machi 2002.

## 3.0 Muhtasari wa Maendeleo Chanya ya Haki za Kibinadamu Tanzania, Novemba, 2021 – Aprili, 2022

### 3.1 Haki za Kiuchumi na Kijamii

Nchi ya Tanzania kwa kiasi imefanya makubwa katika utekelezaji wa haki za kiuchumi na kijamii. Tume inatambua na kupongeza jitihada zilizofikiwa katika kuboresha haki za elimu na afya katika muda huo.

#### a) Haki ya Elimu

Nchi, kupitia Sera ya Serikali imewezesha kurejesha mashuleni wanafunzi wajawazito na Mama wa Watoto mashuleni. Hatua hii ya Serikali imefikiwa ili kurekebisha hali iliyokuwepo ya kuwanyima watoto wa kike haki ya kupata elimu kwa kuwazuia kurejea shuleni baada ya kupata ujauzito. Mabadiliko haya chanya yanaenda sambamba na maendeleo ya kuimarisha na kuboresha miundominu ya sekta ya elimu nchini. Ujenzi wa majengo ya shule unafanyika kote nchini ili kuhakikisha kila mtoto afurahia haki ya elimu. Mwezi Januari, 2022, Serikali ilitangaza kukamilisha ujenzi wa vyuma vya madarasa Elfu Kumi na Tano. Ili kwenda sanjari na hilo Serikali imetangaza kuongeza idadi ya walimu.

#### b) Haki ya Afya

Tume pia inatambua jitihada zilizofanywa na Serikali katika kuimarisha sekta ya afya ikiwa ni pamoja na kujenga vituo vya afya kila Wilaya ili kuwezesha kuwepo kwa huduma za afya zinazofikiwa kwa karibu. Maboresho pia yameonekana katika kupambana na Mviko 19.

#### c) Haki ya Maendeleo

Miradi mikubwa inaendelea katika sekta za mawasiliano; nishati; afya; na usafiri. Kwa ujumla, maboresho haya yatasaidia kuwawezesha wananchi kufurahia haki zao za kijamii na kiuchumi. Serikali imeendelea kutilia mkazo katika uwezeshaji wa kiuchumi wa makundi

yaliyo katika mazingira magumu kama vile vijana, wanawake na walemavu kwa kuzitaka Halmashauri za Wilaya kutenga asilimia kumi ya makusanyo kwa ajili hiyo.

### 3.2 Haki za Kiraia na Kisiasa:

#### a) Haki ya Kushiriki katika Utawala, Uhuru wa Kukusanyika na Kujumuika

Jambo jingine chanya lililoshuhudiwa kutekelezwa ili kuendeleza haki za binadamu ni hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kusawazisha hali ya kisiasa na kiraia nchini. Tarehe 15 Desemba 2022, kwa mfano, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikutana na viongozi wa vyama vya siasa na wadau wengine kujadili hali ya kisiasa nchini. Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa ni uchaguzi huru, haki ya kufanya maandamano; mikutano ya vyama vya siasa; na haki ya uhuru wa kukusanyika. Mkutano huo ulimalizika kwa kuunda Kamati Tendaji ili kuratibu utekelezaji wa mapendekezo ya Mkutano huo.. Hatua nyingine iliyofikiwa ni usajili wa muda wa chama kipya cha siasa mwezi Aprili, 2022.

#### b) Uhuru wa Kujieleza

Kwamba, Tume inapongeza, hatua ya Serikali ya kurekebisha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016; Kanuni za Maudhui ya Mtandaoni; na Kanuni za Redio na Televisheni zitakazoboresha hali ya Uhuru wa kujieleza nchini. Hapo awali, sheria hizi za vyombo vya habari zilimpa Waziri wa Habari mamlaka na busara ya kukemea na kutoa adhabu kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari bila ya kuwa na utaratibu maalumu wa kuthibitisha utovu wa nidhamu unaodaiwa. Hali hii ilikuwa ni kikwazo cha uhuru wa maoni kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

Mwezi Machi, 2022 Baraza la Habari Tanzania liliendesha warsha kuhusu sheria za vyombo vya habari iliyohudhuriwa na wahariri wa Tanzania; waandishi wa habari; vilabu vya vyombo vya habari; vikundi vya haki za binadamu na wadhibiti wa vyombo vya habari vya serikali juu ya changamoto zinazosababishwa na sheria za vyombo vya habari katika

kufanya kazi zao. Mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali yaliwasilishwa wizara husika ili kufanyiwa kazi.

Hatua nyingine chanya iliyofikiwa na Serikali ilikuwa kurejeshwa kwa magazeti manne yaliyopigwa marufuku mnamo Februari, 2022.

### c) Upatikanaji wa Haki

Tume inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya kutaka kuimarisha mfumo wa haki jinai nchini.Hivi karibuni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza Jeshi la Polisi kuacha kuwaonea wananchi na kutumia nguvu nyingi wakati wa kutekeleza majukumu yao badala yake wazingatie sheria, weledi na maadili. Mhe. Rais alielekeza kuwepo mabadiliko ya sheria ya kuweka watu ndani matumizi ya nguvu katika vituo vya Polisi na wakati wa kushughulikia masuala ya haki. Hii ililenga katika kuboresha taratibu za awali wakati wa kushughulikia kesi za jinai kabla ya kuanzisha mashtaka.

Hivi karibuni, Bunge limepitisha marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai yanayohusu vifungu vinavyohusika na kuharakisha upelelezi na kukataza kukamatwa watuhumiwa baada ya kuachiwa huru na mahakama kutokana na kutokamilika kwa upelelezi. Mabadiliko hayo ya Sheria pia yanaondooa kinga ya maafisa na askari wa Jeshi la Polisi kutoshitakiwa kutokana na kutumia madaraka vibaya wakati wa utekelezxaji wa majukumu yao.

Tume inaamini kwamba, maendeleo haya pamoja na maboresho ya hivi karibuni katika usimamizi wa utoaji haki; yatawezesha kuwepo kwa utoaji haki kwa kuzingatia viwango vya kikanda na kimataifa vya haki za binadamu.

## 4.0 Upimaji wa Utekelezaji wa Haki za Binadamu -*UPR*

Tume inatambua kwamba, kwa kuzingatia Ripoti ya *UPR* - Mkutano wa 43, Baraza la Haki za Kibinadamu la Kikao cha 49 cha Kawaida; Serikali ilikubali kutekeleza Mapendekezo 187 (pamoja na 20 yaliyokubaliwa kwa sehemu) kati ya mapendekezo 252 yaliyowasilishwa

kwa Serikali. Hata hivyo mwitikio chanya kwa upande wa Serikali ni kwamba inakusudia kujumuisha mapendekezo yaliyokubaliwa katika Mpangokazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu unaofanyiwa mapitio sasa. Kuingizwa kwa mapendekezo yaliyokubaliwa katika mpango huu wa jumla kutapanua wigo wa kushughulikia masuala ya haki za binadamu nchini na hivyo kuboresha ufanisi wa kuimarisha mfumo wa kitaifa wa ulinzi na uendelezaji wa haki za binadamu kupitia matukio na kazi mahsusi .

## 5.0 Muhtasari wa Matukio Hasi ya Haki za Kibinadamu Novemba 2021 - Aprili 2022

Tume inatambua kwamba kwamba, pamoja na maboresho chanya yaliyotajwa hapo juu, kumekuwa na changamoto kadhaa kuhusu masuala ya haki za binadamu nchini kama ifuatavyo:

a. Wakati ripoti za hivi karibuni zimeonyesha kupungua kwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto (ukatili wa kijinsia na usafirishaji haramu wa watoto hasa Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara mtawalia), changamoto bado inaendelea. Serikali inapaswa kufanya juhudi zaidi kuboresha hali hiyo;'

b. Hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko la matukio ya ukatili na mauaji ya watu wa karibu na wenza katika maeneo mbalimbali yaTanzania Bara. Kwa mfano, katika kipindi cha tarehe 1 hadi 31 Januari, 2022, Jeshi la Polisi liliwashikilia watu 150 kwa tuhuma za kuhusishwa na mauaji hayo. Mauaji hayo yanaendelea licha ya mpango wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuunda Kamati Maalum na kuipa jukumu la kutafuta suluhu ya kukabiliana na hali hiyo; na

c. Zipo changamoto mbalimbali zinazokabili mfumo wa haki Jinai hususani hali ya vizuizi vya mahabusu licha ya maboresho mbalimbali yanayofanywa na Serikali. Katika kuzingatia usafi, seli za magereza na polisi zinahitaji maboresho katika kuhakikisha uwepo wa rasilimali kama vile mataulo ya kike kwa usafi na magodoro ya kulalia. Pia, ubora wa mifumo ya mifereji ya maji taka unahitaji kuboreshwa.

## 6.0 Mapendekezo

Tume inapendekeza yafuatayo:

a. Serikali iendelee na mchakato wa marekebisho ya sheria zinazolalamikiwa, zikiwemo zinazohusu Mfumo wa Haki ya Jinai. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2015; Kanuni za Maudhui ya Mtandaoni, 2020; na, Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi ( *PGOs*), kutaja chache tu;

b. Serikali ihakikishe kwamba watekelezaji wa sheria wanaokiuka haki za binadamu wanawajibishwa. Kwa mfano, Serikali inapaswa kuzingatia uundaji wa chombo huru cha uangalizi wa polisi;

c. Serikali inapaswa kutumia juhudi shirikishi kuongeza uelewa wa umma katika kushughulikia baadhi ya masuala magumu kama vile ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto;

## Hitimisho

Waheshimiwa wajumbe wa Tume ya Afrika ya Haki za Watu na Binadamu (*ACHPR*); wanachama shirikishi; wajumbe mliohudhuria Kikao cha 71 cha *ACHPR*, ninawashukuru kwa mwaliko wenu, na pia ninawashukuru kwa umakini wenu. Nakutakieni mjadala wenye matunda.

**Jaji (Mst.) Mathew P.M. Mwaimu**

**Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tanzania.**

**Aprili 26, 2022.**